



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA**



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

10/03/2023

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imepokea kibali Mbadala kwa Ajira mpya katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 chenye Kumb. Na FA.170/361/01"B"/46 cha tarehe 30 Januari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini.

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI MBILI (2)

1.1. Sifa za Mwombaji:

Muombaji awe amehitimu kidato cha nne au sita na mafunzo ya Stashahada (NTA Level 6) katika fani ya urasimu ramani (cartography) au (geoinformatics), sheria, afya au masjala kutoka vyuo vinavyoambuliwa na Serikali, wenye ujuzi wa kompyuta.

1.2. Majukumu ya Msaidizi Wa Kumbukumbu Daraja La II

- (i) Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye regista (incoming correspondence register)
- (ii) Kuorodhesha barua zinzotoka nje ya taasisi (outgoing correspondence register)
- (iii) Kusambaza majalada kwa watendaji (action officer's)
- (iv) Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa watendaji
- (v) Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji.
- (vi) Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa
- (vii) Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (file tracking).

1.3. Ngazi ya Mshahara

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani **TGS C** kwa mwezi

1.4. Masharti ya Ajira- (Ajira ya kudumu)

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA KILA MWOMBAJI

- (i) Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe na namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa(NIDA)
- (ii) Muombaji awe na umri kati ya miaka 18-45
- (iii) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jina au kufungwa jela.
- (iv) Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji CV.
- (v) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha ndogo (Passport Size) ya hivi karibuni.
- (vi) Testimonial, Result slip, Provisional Result, kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA**
- (vii) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono
- (viii) Waombaji waliosoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganifu na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
- (ix) Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa kazi au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa upya.
- (x) Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi yaani NTA levels maombi yatakayopokelewa na kufanyiwa kazi ni maombi ya cheti ngazi ya NTA Level 6 tu.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **23/03/2023** saa **9:30** Mchana

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga,
S.L.P. 22,
Mahenge/Ulanga
MOROGORO.


Adv. Andreas N. Whero

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
H/W-ULANGA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
ULANGA

Nakala:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320
DODOMA.

-Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
www.ulangadc.go.tz

-Mbao za matangazo